**MULIKA Na. 40(2) 2021 (95-108)**

# Athari za Kimaadili Zitokanazo na Nyimbo za Muziki wa Singeli nchini Tanzania

*Aaron A. Mukandabvute*[1]
Chuo Kikuu cha Zimbabwe
na
*Maria Gores*[2]
Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala nchini Tanzania

## Ikisiri

Kumekuwa na madai kwamba nyimbo za muziki wa singeli zimechangia kuporomosha maadili ya jamii wakati madai mengine yanaona nyimbo hizo za muziki zina dhima muhimu ya kuleta ustawi wa kimaadili kama muziki wa kawaida wenye kutekeleza majukumu muhimu katika jamii. Kutokana na kuhitilifiana kwa wanazuoni kuhusu umuhimu wa nyimbo za muziki za singeli, makala haya yanakusudia kuchunguza ni kwa namna gani nyimbo hizo zinavyoathiri maadili ya jamii. Uchunguzi huu ulifanyika kwa kufuata mikakati anuwai ya kiuhakiki. Kwanza, ilibainishwa kuwa zipo nyimbo za muziki wa singeli zenye athari chanya na pia athari hasi. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa ambapo zililengwa nyimbo za muziki wa singeli zinazobeba athari chanya na hasi katika maadili ya jamii. Uchanganuzi wa data umeongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika na Nadharia ya Muziki Simulizi. Matokeo yanaonesha kwamba nyimbo za muziki wa singeli zinaakisi uhalisi wa matendo adilifu pamoja na matendo yasiyo adilifu yanayotendeka katika jamii ya Waswahili wa Tanzania. Kutokana na ufumbuzi huo, imependekezwa kuwa wasanii wa nyimbo za muziki wa singeli, wanajamii pamoja na taasisi mbalimbali zinazosimamia maadili katika jamii kwa pamoja waendelee kutumia nyimbo za muziki wa singeli kama chombo cha kudumisha maadili na vilevile kukosoa matendo yasiyokubalika katika jamii siyo tu katika jamii ya Waswahili bali hata duniani kote. Imehitimishwa baada ya upembuzi kwamba nyimbo za muziki wa singeli ni kioo cha uhalisia kama matokeo yanavyodhihirisha. Hivyo, makala haya yanashindwa kukubali au kukataa madai kwamba nyimbo za muziki wa singeli ni chanzo cha mmomonyoko wa maadili.

## 1.0 Utangulizi

Makala haya yanahusu namna nyimbo za muziki wa singeli zinavyoathiri maadili ya jamii. Katika kujadlli suala hilo, waandishi alitumia nyimbo nne kutoka kwa wasanii wanne tofauti. Wimbo wa kwanza unaitwa “Utanikumbuka” ulioimbwa na Dogo Zero akishirikiana na Sniper. Wimbo huu unazungumzia changamoto zinazoikumba taasisi ya ndoa. Katika muktadha wa wimbo huu matendo mabaya ya mwanamke yamesawiriwa kama chanzo cha changamoto zinazoikumba ndoa yake. Mwanamke anaambiwa kuwa atamkumbuka mume wake baada ya kuachwa.

[1] **Barua pepe:** *aaroemukanda5151@gmail.com*
[2] **Barua pepe:** *mariagoress@gmail.com*

Wimbo wa pili unaitwa “Wanga” ulioimbwa na Meja Kunta (Mwalami Sadiki) akishirikiana na Lavalava (Abdul Juma Idd). Wasanii wanapingana sana uchawi kwa kuwa hurudisha nyuma maendeleo ya jamii. Aidha, wimbo wa tatu unaitwa ‘Hainaga Ushemeji’ ulioimbwa na Man Fongo (Amani Khamisi). Wimbo huu unamsawiri shemeji kama mtu wa kufanya mapenzi na wanaume wengi. Wimbo wa nne unaitwa “Madanga ya Mke Wangu” ulioimbwa na Meja Kunta na D Voice. Huu ni wimbo juu ya mwanamume anayemtuma mkewe kudanga kama njia ya kupata kipato ili kuwasaidia kujikimu kimaisha. Katika sehemu ifuatayo tunafafanua maoni ya wataalamu, etimolojia ya singeli na dhana ya muziki.

## 1.1 Maoni ya Wataalamu Kuhusu Nyimbo za Muziki wa Singeli

Kama ilivyodokezwa hapo awali, makala haya yanalenga kuchunguza maadili katika nyimbo za muziki wa singeli nchini Tanzania. Singeli ni muziki ibuka ambao kwa sasa ni muziki pendwa hasa kwa kizazi kipya. Kutokana na jinsi watu wanavyoucheza muziki huu, kumekuwa na madai kwamba nyimbo za muziki wa singeli huenda kinyume na maadili yanayotarajiwa katika jamii. Hivyo, jamii imekuwa ikiutazama muziki wa singeli kwa mitazamo inayokinzana (http://www.mtaakwamtaa.co.tz/2019/08/meja-kunta-awaomba-wasanii-wa-singeli.html).

Katika mtazamo wa kwanza kumekuwa na madai hasa katika mitandao ya kijamii kwamba nyimbo za muziki wa singeli zimekuwa zikichochea mmomonyoko wa maadili na matokeo yake kusababisha matendo yasiyo adilifu yaliyokithiri katika jamii. Watetezi wa madai haya wanaeleza kuwa, sababu ya msingi ni kwamba nyimbo hizo ndizo zimekuwa zikiwatia hamasa wanajamii kuiga matendo yasiyofaa kama wanavyoyaona kwenye video, picha na kuyasikia mashairi ya nyimbo hizo.

Katika mtazamo wa pili, kuna watu wanaona nyimbo za muziki wa singeli kwa mtazamo tofauti. Waungaji mkono wa hoja hii wanafananisha nyimbo za muziki wa singeli na aina nyingine za muziki ambazo lengo na dhima yake ni kumburudisha msikilizaji (https://pan-african-music.com/en/singeli-the-future-sound-of-tanzania). Kutokana na mkinzano huu, makala haya yanalenga kuchunguza suala la maadili katika mashairi na video za nyimbo za muziki wa singeli. Zahoro (2018) akiangalia vionjo vya fasihi ya kisasa ya Kiswahili katika nyimbo teule za singeli, anabainisha kuwa nyimbo za muziki wa singeli zina athari hasi na chanya katika maadili ya jamii. Uchunguzi wa Zahoro (2018) unajikita katika mashairi tu ya nyimbo teule lakini makala haya yanakusudia kuchunguza maadili katika mashairi pamoja na video za nyimbo za muziki wa singeli. Aidha, kutokana na ukuruba uliopo baina ya nyimbo, muziki na utendaji wa singeli, sehemu ifuatayo inaelezea kwa ufupi dhana ya muziki, na dhima yake katika jamii.

## 1.2 Dhana ya Muziki

Muziki ni sanaa ambayo huhusisha sauti zilizopangwa katika mpangilio maalumu zenye kusikika (Mapuwei na Kemunto, 2013). Katika mkondo huo, Zahoro (2018:2) anafafanua muziki kama ifuatavyo:

> Muziki ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki au wizani.

Hivyo, ni bayana kuwa muziki ni utanzu wa sanaa ambao huwasilishwa kupitia uimbaji. Kutokana na mpangilio maalumu wa mapigo, muziki huweza kupigwa kwa kutumia ala mbalimbali za muziki. Vilevile, nyimbo na muziki huweza kuwa na uhusiano kwani nazo hutumi lugha teule na huhusisha kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti.

**1.3 Nyimbo za Muziki wa Singeli: Etimolojia yake**

Nyimbo za muziki wa singeli ni aina ya muziki maarufu sana maeneo ya Pwani katika makazi ya Waswahili nchini Tanzania. Muziki huu ni mchanganyiko wa ladha ya taarabu, bongo fleva na mchiriku na pia huchukuliwa kama 'mnanda' wa kisasa (BBC News Swahili, 2016). Mabadiliko ya wakati yamechangia mabadiliko katika nyimbo asili na kuibua aina nyingine ya muziki kama vile singeli (Zahoro, 2018). Kwa mantiki hii, nyimbo za muziki wa singeli huweza kupigwa kimdundiko, kimchiriku, kivanga, kimnanda na kitaarabu. Pia, nyimbo hizi huchombezwa kwa maneno mbalimbali kama vile kutaja majina ya sehemu mbalimbali na majina ya watu ili kutoa shukrani kwa mtu aliyemsaidia msanii kwa jambo lolote kama vile kumpa wazo la wimbo, kumsaidia fedha za kulipia studio ili arekodi wimbo wake au kumuandikia mashairi ya wimbo. Nyimbo za muziki wa singeli zimekuwa zikipigwa katika shughulli mbalimbali, mathalani, kwenye harusi, Maulid, kumtoa mtoto, ndoa na sikukuu za kidini kwa kutaja chache. Vilevile, nyimbo hizi zimekuwa na kushika kasi hususani jijini Dar es Salaam ambapo kuna wasanii wengi wanaoimba muziki huu na kupata umaarufu mkubwa sana hasa kwa vijana.

Nchini Tanzania, takribani asilimia 66.8 ya Watanzania wanaufahamu muziki huu na wanausikiliza kwa njia tofautitofauti, mathalani, kwenye simu, redio pamoja na kuupiga kwenye sherehe mbalimbali (https://www.bbc.com/swahili/habari-37135137). Aidha, katika sherehe mbalimbali, nyimbo za muziki wa singeli ndizo zinazopigwa sana ikilinganishwa na aina nyingine ya muziki wa Kitanzania kama vile bongo fleva, hiphop na nyimbo za Injili. Hivyo, kutokana na umaarufu wake kwa wasikilizaji wengi, nyimbo hizi zimekuwa mojawapo ya mitindo pendwa ya muziki au muziki unaotamba nchini Tanzania. Nyimbo za muziki wa singeli zilianza na wasanii wachache sana. Msanii aliyekuwa mwasisi na kusikika sana alikuwa Msaga Sumu (Selemani Jabir Msonjele) aliyejulikana kwa nyimbo zake zilizotamba katika kipindi hicho na bado zinaendelea kutamba, kwa mfano, wimbo wa "Naipenda Simba".

**2.0 Methodolojia**

Mkabala uliotumika katika uandishi wa makala haya ni wa kimaelezo kutokana na uhitaji wa mada husika kwani kwa kiasi kikubwa makala haya yamehusisha maelezo juu ya mashairi na video za nyimbo teule.

Data ya utafiti ilikusanywa kutoka kwenye mtandao wa *You Tube* kwa kutumia usampulishaji lengwa. Kwanza, usampulishaji lengwa ulitumika ambapo ziliteuliwa nyimbo nne za muziki wa aina ya singeli na wala siyo aina nyingine ya muziki. Pili, katika sampuli ya nyimbo nne zilizoteuliwa, data zilizolengwa ni mashairi pamoja na video. Tatu, katika nyimbo teule, mbili zilikusudiwa kubeba mashairi na video

zinazoakisi matendo adilifu kwa kiasi kikubwa na nyingine mbili zilikusudiwa kubeba mashairi na video zinazoakisi matendo yasiyo adilifu kwa kiasi kikubwa.

Aidha, mashairi ya nyimbo teule yaliandikwa na uchanganuzi wake ulifanyika kupitia mbinu ya uchambuzi matini. Video ziliangaliwa zikachambuliwa kupitia mbinu ya ushuhudiaji wa matendo yanayotendeka kwenye video. Kutokana na ufinyu wa muda, sehemu za video zilizochunguzwa ni zile tu zinazoendana na ubeti wa mashairi husika, ili kupata picha toshelevu ya kile kinachoimbwa na matendo yanayotendeka kwenye video wakati huohuo.

Uchanganuzi wa data uliongozwa na nadharia mbili ambazo ni Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika iliyoasisiwa na Sengo (1970) pamoja na Nadharia ya Muziki Simulizi iliyoasisiwa na Almen (2009). Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika inasisitiza kuwa jamii za Kiafrika zimejengwa katika mazingira halisi ambayo kuna mambo halisi yanayofanyika na kukubalika kwa Waafrika (Kisanji, 2013).

Vilevile, Nadharia ya Muziki Simulizi inadai kwamba muziki ni chombo kitumikacho kuwasilisha mambo yanayofungamana na maisha ya binadamu kama vile wakati na mabadiliko. Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika ilitumika katika uchunguzi wa matendo yaliyomo kwenye video za nyimbo teule ili kueleza nini kilichokuwa kinatendeka. Mathalani, Nadharia ya Muziki Simulizi ilitumika katika kusimulia matendo yaliyotendeka katika mashairi ya nyimbo zilizoteuliwa. Nadharia zote mbili zilisaidia katika uchunguzi wa matendo yaliyobebwa kwenye mashairi pamoja na video kuhusiana na maadili.

## 3.0 Matokeo ya Utafiti na Uwasilishaji wa Data

Makala haya yalilenga kuchunguza jinsi ambavyo nyimbo za muziki wa singeli zinavyoathiri suala la maadili katika jami ya Watanzania. Matokeo yanaonesha kwamba nyimbo za muziki wa singeli zinahamasisha maadili mema na wakati huo huo zinahamasisha maadili yasiyo mema. Baada ya uchunguzi wetu imedhihirika kuwa wasanii wametumia sanaa hii kama chombo cha kuhamasisha, kuasa, kuadabisha na kuonya jamii juu ya masuala mtambuka yanayoiathiri jamii kila kukicha. Aidha, uchunguzi umebainisha kwamba wasanii wametumia sanaa ileile kuchochea athari zinazokwenda kinyume na maadili yanayoendana na utamaduni wa Mtanzania. Tutaanza na kuchunguza athari chanya tulizozibaini kutoka katika nyimbo mbili ambazo ni ‘Utanikumbuka’ na ‘Wanga Wabaya’.

### 3.1 Athari Chanya za Kimaadili katika nyimbo Zilizochunguzwa

Kutokana na data za makala haya, imebainika kuwa kuna athari chanya zinazopatikana kutoka katika mashairi na video za nyimbo za muziki wa singeli. Athari hizo ni kukemea ushirikina na uchawi, kudumisha umoja, umuhimu wa salamu, kupinga tabia ya kuzua uongo au kusema uongo, kupinga matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, nafasi ya mwanamume na mwanamke katika ndoa na haki ya mapenzi. Sehemu inayofuata imefafanua athari hizi kama ifuatavyo.

#### 3.1.1 Kukemea Ushirikina na Uchawi

Mara nyingi, imani za kishirikina na uchawi ni tatizo linaloikumba jamii pamoja na kurudisha nyuma maendeleo kwa namna moja ama nyingine. Wakati mwingine, hali hii hutokana na baadhi ya wanajamii kumwonea wivu aliyepata maendeleo, hivyo, wanamfanyia ushirikina ili apoteze kile alichokipata. Uchambuzi wa nyimbo za

muziki wa singeli umedhihirisha kuwa wasanii wa singeli hukemea ushirikina na uchawi. Katika ubeti wa tatu wa shairi la "Wanga" Meja Kunta na Lavalava wana haya ya kusema katika ubeti huo:

(1)

*Ukiwa nacho watakuroga wanga*
*Ukiwa hauna watakuroga wanga*
*Ukipata pesa watazusha unadanga*
*Wakati mwenyewe unajichanga*

Hapa tunaona kuwa wasanii wametunga mashairi kisanii wakionesha kuwa wachawi watakuroga pale unapopata maendeleo. Pia, wachawi wanazusha mtu amepata maendeleo kupitia njia siziso sahihi kama vile umalaya wakati mtu amejikwamua kwa jasho lake. Hii inadhihirisha kwamba suala la uchawi lipo katika jamii za Waafrika japokuwa siyo watu wote wanaukubali.

Aidha, katika ubeti huo video inaonesha wachawi watatu waliofumaniwa ambao ni wanaume wawili na mwanamke mmoja. Wachawi hao wanaonekana wameketi chini kwa aibu sana wakati wamezungukwa na umati wa watu na kukemewa. Kutokana na hali hiyo inabainika kuwa uchawi ni jambo lisilokubalika kamwe katika jamii na ni jambo la kuaibisha.

### 3.1.2 Kudumisha Umoja

Umoja ni nguvu ilhali utengano ni udhaifu. Hali kadhalika, matunda ya umoja ni amani na utulivu ambavyo huwezesha maendeleo endelevu katika kujenga jamii. Kwa mujibu wa United Nations (2019) ni azimio la kila jamii duniani kudumisha umoja na utulivu ili kuhakikisha maendeleo endelevu. Katika shairi la "Wanga" wasanii wamesisitiza yafuatayo juu ya umoja katika ubeti wa sita. Wanasema:

(2)

*Labda nami nifanye kipi kizuri waja*
*Niwe rafiki wa kila mja*
*Iwe furaha inishinde husda*
*Haya yapite mengine yaja*

Katika mistari hii, tunaona kuwa wasanii wameweka msisitizo katika kudumisha umoja japokuwa watu wengine wanakuwa na husda inayosababisha utengano na kutokuelewana baina yao. Kwa mantiki hiyo, wasanii wanawaasa wasikilizaji juu ya umuhimu wa umoja na kuonesha kuwa suala la umoja linafungamana na maisha ya mwanadamu.

Mathalani, katika ubeti huu bado video inatuonesha wale wachawi wameketi chini lakini sasa wanazungukwa na watu wanaocheza ngoma. Pia, msanii yupo katikati ya wale wachezaji akiimba kwa sura ya huzuni sana huku akirusha mikono juu. Inabainika kuwa msanii yupo katika hali ya kuumia roho kutokana na tukio la wachawi lililotendeka. Hivyo, tunaweza kusema kuwa uchawi ni jambo ambalo lipo ingawa linaumiza, linasikitisha sana na halipaswi kutendeka katika jamii.

### 7.1.3 Umuhimu wa Salamu

Salamu ni kipengele cha kitamaduni ambacho hutumika katika tamaduni zote kumjulia mtu hali. Ni sehemu ya mawasiliano ya binadamu ambayo hulenga kujenga uhusiano mwema miongoni mwa wanadamu wanapotagusana kimaneno na kiishara

mwili (Ngugi; 2014). Katika ubeti wa nane wa shairi la 'Wanga' Meja Kunta na Lavalava wanasema:

(3)

*Wapi DJ Juck, msalimie sana P masta*
*Wanangu wa Bunju, wanangu wa Bunju*
*Kilaini mpe salamu mzee Pwagu*
*Mwambie bado napambana heheeee*
*This is Mr Love bite, ninja Kumfu Masta Shivo*

Mistari hii inaonesha jinsi ambavyo msanii wa singeli anavyoshirikiana na jamii yake, anawaamkia marafiki zake pamoja na wezee. Katika jamii hususani ya Waswahili, suala la salamu huchukuliwa kwa namna ya pekee sana kiasi kwamba usipotoa salamu kabla huwezi kupata huduma. Ni sahihi kusema kuwa shairi hili linaendelea kudumisha salamu kama ilivyo desturi ya jamii.

Pamoja na hayo, video inaonesha wasanii, wachezaji pamoja na wapiga baragumu katika hali ya furaha. Wale wachawi hawapo katika sehemu hii ya video. Kila wakati mwimbaji anapotoa salamu baragumu zinapigwa. Tunabaini kuwa salamu hutolewa katika hali ya furaha kama ilivyo mila na desturi za Waafrika. Aghalabu, nyimbo za muziki wa singeli hufungamana na salamu (Zahoro, 2018).

### 3.1.4 Kupinga Tabia ya Kuzua Mambo au Kusema Uongo

Kusingiziwa huweza kusababisha mtafaruku, ugomvi au hata vifo kwa wanajamii kutegemeana na kitendo husika ambacho mtu amesingiziwa. Mtu anaposingiziwa kufanya jambo ambalo hajalifanya au halijafanyika, kwanza, yeye mwenyewe huweza kuathirika pamoja na watu wanaomzunguka. Katika ubeti wa tano, Meja Kunta na Lavalava wanalalamika:

(4)

*Hata mimi yalinikuta*
*Nikasingiziwa nimekufa*
*Mama yangu alilia sana*
*Ooo! Ooh! Huruma mama*

Katika mistari hii, tunaona kuwa wasanii wameibua suala la kusingiziwa uongo kisha wakamwonesha msikilizaji madhara yake ambapo mama mzazi alilia sana aliposikia kuwa mwanaye amefariki. Hali hii inadhihirisha kuwa suala hilo hutokea katika jamii za Waafrika. Aidha, video inatuonesha msanii amemshika shingoni mchawi mmoja wa kiume akimwangalia machoni kwa huzuni. Anaonekana anamwuliza swali lakini yule mchawi anabaki ameshangaa. Sehemu hii ya video inadhihirisha kuwa uzushi unaofanywa na wachawi hauna sababu za msingi kama yule mchawi anavyokosa majibu ya kile anachoulizwa.

### 3.1.5 Kupinga Matumizi Mabaya ya Mitandao ya Kijamii

Siku za hivi karibuni matumizi ya mitandao ya kijamii yamekithiri kutokana na utandawazi na maendeleo ya kiteknolojia. Mathalani, kwa upande wa wasanii, mitandao ya kijamii imekuwa pia uwanja wa kujinadi kwa kurusha picha, video, ujumbe na kadhalika ili kuendeleza kazi zao. Hata hivyo, ingawa mitandao ya kijamii imekuwa na manufaa katika fani hii, imechochea pia matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii kama vile kutukana matusi, ugomvi na wivu (Obiri na Lutta, 2015). Katika

ubeti wa saba, wasanii wanaibua na kukemea suala la matumizi mabaya ya mtandao katika mistari ifuatayo:

(5)

*Mbona wana mambo meusi*
*Nikiposti picha wanacomment matusi*
*Nikikonda tu una virusi*
*Wana roho za kenge mixer mijusi (Mscheew)*

Katika mistari hii tunaona kuwa msanii amekosoa pamoja na kupinga matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii kwa ujumla. Hivyo, mashairi haya yanakosoa matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii. Ukosoaji huu unadhihirika pia kwenye video katika ubeti huu ambapo mwimbaji amejishika mikono kwa masikitiko akikemea kitendo hiki. Kwa mantiki hiyo, wasanii hawa wametumia sanaa yao kutuonesha kuwa matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii yapo na hayapaswi kuungwa mkono kwa namna yoyote.

### 3.1.6 Nafasi ya Mwanamke na Mwanamume katika Ndoa

Ndoa ni taasisi muhimu katika maisha ya binadamu. Hii ni mojawapo ya asasi zinazohakikisha kuijenga familia pamoja na kukua na kuendelea kwa jamii (Gicuku, 2011). Hata hivyo, asasi ya ndoa imekumbwa na changamoto anuwai tangu mwanzo wake. Changamoto hizi zimekuwa na matokeo mabaya mpaka hata kuvunjika kwa ndoa. Kutokana na maelezo tangulizi, tunaona kwamba changamoto za ndoa zina madhara mabaya katika ujenzi na maendeleo katika familia pamoja na jamii. Katika shairi la "Utanikumbuka", wasanii wameangazia changamoto mbalimbali zinazoikumba asasi ya ndoa, ikiwemo nafasi ya mwanamke na mwanamume kwenye ndoa. Katika korasi ya shairi hili mwanamke anaulizwa maswali yafuatayo:

(6)

*Kwani humu ndani mwanaume nani?*
*Kwani humu ndani mwanamke nani?*
*Kwani humu ndani kaolewa nani?*
*Kwani mapenzi kayaleta nani?*

Katika mistari hii, wasanii wamesuka shairi kisanii wakiuliza maswali ya kumfikirisha msikilizaji juu ya kutambua nafasi ya mwanamke na mwanamume katika ndoa. Kwenye video, mwanamume anamwuliza maswali yote haya wakati mke wake ambaye anaendelea kujiremba kwenye kioo huku akionesha sura ya dharau. Kwa kuzingatia muktadha wa wimbo huu, wasanii wameamua kumchora mwanamke asiyetambua nafasi yake katika ndoa na kuibua ugomvi unaoendelea. Katika jamii ya Watanzania na Waafrika kwa ujumla, mgawanyo wa kimajukumu umepambanua majukumu ya mwanamke na mwanamume katika ndoa. Katika jamii yenye kufuata mfumo wa maisha ujulikano kama mfumo dume, mwanamke hufanya majukumu ya ndani wakati mwanamume hufanya majukumu ya nje (Massoud, 2018). Hapa mwanamume anaendelea kuuliza yafuatayo katika ubeti wa tatu wa shairi:

(7)

*Haya deki kapiga nani jana?*
*Vyombo kaosha nani jana?*
*Na michupi kafua nani jana?*
*Na nywele zako kakusuka nani jana?*
*Mbona hueleweki jamani mama?*
*Unakojoa kitandani mama*

*Hivi unanitesa kitu gani mama?*
*Heshima ya mume iko wapi bwana?*

Kwa mujibu wa mila na desturi za Kiafrika ni dhahiri kuwa mwanamke ameshindwa kutambua nafasi yake katika ndoa hadi mwanamume anaanza kufanya kazi za ndani kama kupiga deki, kuosha vyombo na kumsuka nywele mke wake. Majukumu haya yanatarajiwa kufanywa na mwanamke katika jamii ya Waafrika kutokana na mfumo uliowekwa na jamii hii. Hivyo basi, shairi linaendelea kumkumbusha msikilizaji kuwa katika jamii zetu, hususani za Kiafrika, kazi hizi zinatarajiwa kufanywa na mwanamke wakati mwanamume akitafuta kipato nje ili kuilisha familia. Pamoja na hayo, video inamwonesha mwanamke akimtupia mume wake chupi ili afue. Tunaona pia mwanamume anafanya jukumu lake la kuuza matunda na huku mkewe anazurura mtaani. Kwa mantiki hiyo, mwanamke anashindwa kutimiza majukumu yake wakati mwanamume anafanya yake. Hivyo, wimbo huu unaionesha jamii kuwa kila mmoja anatakiwa kutimizaa majukumu yake katika ndoaa naa familia kwa ujumla.

**3.1.7 Haki ya Mapenzi**

Makala haya yamebaini kuwa wasanii wa singeli hutetea na kudai haki ya mapenzi katika ndoa. Ni mojawapo ya wajibu wa wanandoa kufurahishana kimapenzi kwani hilo ni hitajio muhimu la kisaikolojia. Ukosefu wa haki hii umekuwa pigo kubwa katika ndoa nyingi kwani mmoja wao asipopata haki yake huchepuka na hata kusababisha ndoa kuvunjika. Shairi la 'Utanikumbuka' limeibua suala hili kwa kumchora mwanamke anayemnyima mume wake haki ya mapenzi, hivyo, kusababisha kutokuelewana ndani ya nyumba. Katika ubeti wa pili, msanii anauliza pamoja na kulalamika:

(8)

*Mbona wenzangu wanapata madikodiko?*
*Mimi nyumbani kila siku mitikisiko*
*Kisimani anapata madikodiko*
*Mimi nyumbani kila siku mitikisiko*
*Umefundwa na kungwi gani wee mama?*
*Mbona kila siku mitihani wee mama?*
*Umechezwa na ngoma gani wee mama?*
*Mbona mie sikuelewi wee mama?*
*Ona Wana injoy mama wana injoy*
*Wanainjoy Lakini mimi siinjoy*
*Wenzangu waninjoy mama wanainjoyi*
*Wana injoy lakini mimi siinjoy*

Katika mistari hii tunaona kuwa wimbo wa 'Utanikumbuka' unaonesha kwamba asasi ya ndoa imekumbwa na changamoto ya ukosefu wa haki ya mapenzi na furaha. Wasanii wamemchora mwanamume aliyenyimwa haki yake akiwaonea wivu wenzake wanaofurahishwa na wake zao bila ugomvi. Sambamba na hayo, tunamwona kisimani analishwa na mke na hata kubebwa mgongoni wakifanya michezo ya kimapenzi. Kutokana na uchunguzi huu, ni sahihi kusema kuwa shairi na video hii vinaifundisha hadhira juu ya haki ya mapenzi katika ndoa. Pia, mambo hayo yanatokea katika jamii zetu za Waafrika. Kutokana na hoja zilizoelezwa katika sehemu iliyopita, zimedhihirisha kuwa nyinmbo za muziki wa singeli huweza kutumika katika jamii kwa lengo la kuasa, kuonya na kuelimisha jamii katika matendo yasiyofaa. Hivyo

basi, ni muhimu kwa jamii kuziangalia nyimbo hizi kwa mrengo chanya ili zitimize majukumu yake katika jamii.

### 3.2 Athari Hasi za Kimaadili Zitokanazo na Nyimbo Zilizochunguzwa

Kipengele hiki kimechunguza kwa umakini athari hasi zinazosababishwa na nyimbo za Muziki wa singeli. Ingawa wasanii wa singeli wanakosoa matendo mabaya yanayofanyika katika jamii, wanayashabikia na kiasi cha kuonekana kuwa wao wameyaacha bila kuyakosoa. Hivyo, muziki huu humwacha msikilizaji katika hali ile ile ya kushabikia matendo yanayokwenda kinyume na maadili. Zifuatazo ni athari hasi tulizozibainisha: kuhamasisha uzinzi, unyanyasaji wa kijinsia, ujigambaji usio na maana, kuchochea ugomvi na kulipiza kisasi katika nyimbo mbili ambazo ni "Hainaga Ushemeji" na "Madanga ya Mke Wangu".

#### 3.2.1 Kuhamasisha Uzinzi

Uchunguzi umebaini kwamba wasanii wa singeli wanahamasisha uzinzi kwa wasikilizaji. Uzinzi umekuwa pingamizi katika maendeleo ya jamii kwani husambaza magonjwa ya zinaa hususani UKIMWI. Wakati dunia inapambana na janga sugu la UKIMWI, maendeleo endelevu yamekuwa yakikwamishwa pia na janga la UKIMWI (United Nations, 2019). Suala la uzinzi limetupiwa jicho katika nyimbo za muziki wa singeli, kwa mfano, katika shairi la "Hainaga Ushemeji" ubeti wa pili, Manfongo anasema:

(9)

*Wanangu zamu ya nani leo*
*Zamu ya Man Fongo*
*Zamu yako itakuja kesho*
*Usijali baharia wangu*
*Zamu ya nani leo*
*Zamu ya Man Fongo*
*Zamu yako itakuja kesho*
*Usinune baharia wangu*
*Na Meseni kapita*
*Kimeka kapita na*
*Tito kapita*
*Na mpaka B kapita*

Katika mistari hii tunaona vijana wa kiume wakipeana zamu ya kwenda kufanya mapenzi na mwanamke mmoja ambaye ni shemeji yao. Msanii anatumia neno "baharia" kurejelea vijana hawa ambao wanashabikia kitendo wanachokifanya. Pia, katika ubeti huu, video inaonesha vijana wametulia kijiweni mara shemeji anapita kisha wale vijana wanahamasishana kila mmoja wao atapata zamu ya kufanya mapenzi naye. Ujumbe tunaoupata hapa ni uhamasishwaji wa hadhira kuwa hakuna ubaya wowote kufanya mapenzi na mke wa mtu. Kitendo hiki huenda kinyume na maadili ya jamii. Si wimbo wa "Hainaga Ushemeji" tu unaoonekana kuhamasisha uzinzi, bali suala hili linajitokeza pia katika shairi la "Madanga ya Mke Wangu". Katika korasi, Meja Kunta na D Voice wanasema:

(10)

*Naheshimu madanga ya mke wangu*
*Maana ndio yanayonifanya nashiba*

*Naheshimu madanga ya mke wangu mimi*
*Ndo yanayofanya navimba*
*Eeh madanga ya mke wangu*
*Maana ndio yanayonifanya naringa*
*Madanga ya mke wangu yananipa faida*

Katika mistari hii, tunaona kuwa mwanaume anamtuma mkewe kufanya biashara ya kujiuza kimapenzi ili wapate faida ya pesa. Sambamba na mistari hii, katika video mwanaume anaingia ndani kwake wakati mkewe yumo ndani na mteja. Mwanaume anasubiria nje, baadaye mteja anatoka nje akiwa amembeba yule mwanamke. Yote haya baba mwenye nyumba anayashuhudia machoni na kitendo hiki hakimtii wasiwasi. Hivyo basi, tunabaini kuwa suala la uzinzi limechukuliwa kama jambo la kawaida katika wimbo huu, hivyo hadhira nayo itahamasishwa kufanya jambo hili. Aidha, tukiangazia katika jamii za Waafrika mambo haya ya uzinzi (kudanga) yapo na yanatendeka lakini hakuna onyo linalotolewa kwa wahusika kwani inaonekama kama jambo la kawaida.

**3.2.2 Unyanyasaji wa Kijinsia**

Imebainika pia kwamba, nyimbo za muziki wa singeli unahamasisha unyanyasaji wa kijinsia hususani kwa upande wa wanawake. Unyanyasaji wa wanawake umekuwa ukiendelea tangu zama za kale na umekuwa ukijitokeza katika sura mbalimbali. Ingawa jambo hili huonekana kukubalika katika jamii, limepigwa marufuku katika sheria na desturi za kimataifa (Bevilaqua na wenzake, 2010). Katika kiitikio cha shairi la “Hainaga Ushemeji”, Man Fongo anaibua suala hili akisema:

(11)

*Nasikia hainaga ushemeji tunakula*
*Nasikia hainaga ushemeji tunakulaga*
*Nasikia hainaga ushemeji tunakula*
*Nasikia hainaga ushemeji tunakulaga*

Mistari hii inadhirisha kuwa hakuna ubaya wowote kufanya mapenzi na shemeji, ambaye ni mwanamke katika wimbo huu. Katika ubeti huu, mwimbaji anajifanya anakula kitu mdomoni. Hivyo basi, tunabaini pia kuwa mwanamke amechukuliwa kama kiumbe duni na kumfanya kama chombo cha ngono ambacho kila atakaye kujiridhisha kimapenzi anamwendea shemeji. Naye Meja Kunta na D Voice katika shairi la “Madanga ya Mke Wangu” ubeti wa pili wanasema:

(12)

*Kesho usije kurudi bila hela*
*Sa baby ngoja nikuambie*
*Nenda kadange upate kigari tuwavimbie*
*Ooh baby ngoja nikuambie*
*Nenda kadange upate kigari tuwavimbie*
*Halafu home usirudi mapema*
*Usicheze na kazi ma mtu utachina*
*Kwani madanga ndugu hayajatema*
*Mi nimemiss kula chips na nyama*
*Kama ukipata bwana wa kizungu*
*Nenda naye kwa Mpalange*
*Mi mumeo nimekuruhusu kadange*

Mistari hii inaonesha kuwa wasanii wanaibua suala ambalo linamsawiri mwanamke kama kiumbe duni. Badala ya kufanya kazi, mwanamume anamtumia mkewe kama chombo cha kutafutia kipato kupitia umalaya. Video inatuonesha mwanamume amekumbuka 'chipsi' na nyama kwa hiyo anambembeleza mkewe aende kujiuza mwili wake. Hivyo basi, inatosha kusema kwamba huu ni unyanyaswaji wa mwanamke katika ndoa. Aidha, wasanii wanaonekana kulishabikia jambo hili kwani hawajalikosoa kabisa na hali hii huifanya hadhira isione ubaya wowote katika unyanyasaji wa mwanamke na kutokuzingatia usawa wa kijinsia. Mambo hayo katika jamii yapo na hayakemewi.

### 3.2.3 Ujigambaji Usio na Maana

Kuonesha ufahari /kujigamba kwa mambo yasiyo na maana katika jamii huweza kujitokeza. Waswahili husema 'kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza'. Msemo huu umetokana na watu kutafuta sifa za lazima kwa mambo wanayoyafanya yasiyohitaji sifa hizo. Kwa mantiki hiyo, kila mtu katika jamii anatakiwa kujiamini kwa jinsi alivyo na aache sifa zimfuate ikiwa kuna ulazima. Katika wimbo huu msanii anajigamba kwa mambo yasiyoleta maendeleo yoyote kwa jamii. Hata hivyo, hali hiyo inatokana na kutokuwa na heshima na wanawake. Hapa anasema:

*(13)*

*Man Fongo natamba*
*Mtaalamu wa kulamba nguo za mitumba*
*Nitaendelea kutamba*
*Januari mpaka Disemba*
*Natamba natamba wewe mwenyewe si unajua*
*Na kama nyota haing'ai chini ya jua*
*Wanapakazia na maneno wanaponda*
*Maneno maneno hayanizushii kidonda*

Katika mistari hii msanii anaonesha jamii kuwa suala la kujionesha mbele za watu ni jambo la kawaida kitu ambacho siyo kizuri kabisa. Kwenye video, msanii na wachezaji wake wanafanya miondoko ya maringo ili kuendana na ujigambaji. Kila mmoja katika jamii ana namna yake ya kuishi, hivyo mtu anapojigamba mbele ya wengine huweza kuathiri watu wengine kimtazamo hasa kama anajigamba kwa mambo yasiyo na maadili kwa jamii husika.

### 3.2.4 Kuchochea Ugomvi

Imebainika kwamba wasanii wa singeli wamejadili suala la ugomvi linaloibuka katika wimbo wa 'Hainaga Ushemeji' ambapo huweza kuleta machafuko, ugomvi au hata mgawanyiko katika jamii. Suala hili halitakiwi kuchukuliwa kama jambo la kawaida bali jamii inapaswa kulikemea na kuepukana nalo kwa njia moja ama nyingine. Katika nyimbo za singeli zilizochunguzwa tunaona msanii anachochea watu waone suala la unafiki kuwa la kawaida ingawa ni kitu ambacho kinaweza kuleta athari hasi katika jamii. Hapa msanii anasema:

*(14)*

*Binadamu bwana*
*Ukikaa nao hawaishi kukusifia*
*Ukiwapa kichogo kwa nyuma wanakandia*
*Kwani bado hujajua na kama unajua inabii kuwazoea*
*Na kama unajua inabidi kuwazoea*

Hapa msanii anajaribu kutuambia kuwa katika jamii yoyote ile huwa kuna wanafiki ambapo ukiwa nao karibu wanakuongelea vizuri lakini ukiondoka wanakusema vibaya. Kwa mantiki hiyo, wasanii walitakiwa kukemea jambo hilo lakini wao wanasisitiza kuliona la kawaida na kuwazoea watu wa aina hiyo.

### 3.2.5 Kulipiza Kisasi

Kitendo cha kulipiza kisasi kwa watu waliokosea s jambo jema katika jamii hivyo ni athari hasi inayotokana na wimbo huu. Kwa kuwa muziki unawafikia watu wengi zaidi na kwa muda mfupi, dhima kubwa ingekuwa ni kuonya na kukemea mambo mabaya katika jamii. Ikiwa muziki unalenga kuibomoa jamii, hivyo basi jamiii itaathirika kwa kiasi kikubwa kama tunavyoona katika wimbo huu. Msanii ansema:

*(15)*

*Wanangu dawa ya moto moto*
*Man Fongo moto moto*
*Ni dawa ya moto moto*
*G Maker moto tena*
*Dawa ya moto moto*
*Man Fongo moto moto*
*Dawa ya moto moto*
*Man Fongo moto moto*
*Ni dawa ya moto moto*
*G Maker moto tena*

Mistari ya wimbo huu inahamasisha wanajamii kulipiza kisasi. Hali hii haikubaliki kabisa katika jamii kwani huweza kuleta madhara makubwa zaidi. Wahenga walisema ‘usilipize baya kwa baya’. Ikiwa wasanii ambao ndio vioo vya jamii wanasisitiza watu kulipiza kisasi, basi jamii ikifuata mwenendo huo ipotoea na kuhatarisha maisha ya watu wake. Aidha, matendo yanayokwenda sambamba na mistari hii kwenye video yanaonesha kitu kingine, mwanamke na mwanamume wanapita njiani halafu kijana mmoja anakodolea macho makalio ya yule mwanamke. Mumewe analigundua hilo kisha anamsitiri mkewe kwa mwavuli. Katika muktadha mwingine, kikundi cha vijana kinamfuatilia shemeji njiani huku wakitoa macho ya uzinzi. Kwa mujibu wa nadharia zilizotumika, wasanii wanapaswa kutumia nafasi waliyonayo kukemea mambo kama hayo ili jamii iweze kujifunza kutoka kwao.

## 4.0 Hitimisho

Makala haya yamejadili athari za kimaadili zitokanazo na nyimbo za muziki wa singeli. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa nyimbo za muziki wa singeli ni chombo cha msingi katika kuendeleza maadili mema katika jamii kwani huelimisha, hufunza, huasa na hudumisha maadili. Wakati huo huo, imebainika pia kwamba nyimbo za muziki wa singeli huipotosha jamii kwa kushabikia matendo yanayokwenda kinyume na maadili. Kwa maneno mengine, ni dhahiri kuwa muziki una athari chanya na hasi katika maadili ya jamii kutokana na matokeo yaliyobainika. Kutokana na matokeo yaliyopatikana, mwandishi wa makala haya anapendekeza kuwa wasanii wa nyimbo za muziki wa singeli wanapaswa kusimamia na kudai maadili na vilevile kukosoa na kupinga matendo yanayokwenda kinyume na maadili ya jamii. Aidha, inapendekezwa kwamba taasisi mbalimbali zinazosimamia uadilifu katika jamii ziendelee kutumia muziki, hususani singeli kama silaha ya kutetea uadilifu siyo tu katika jamii ya Waswahili bali na duniani kote. Pia, inapendekezwa kwamba mamlaka ya utangazaji nchini Tanzania iendelee kusimamia nyimbo za muziki wa singeli hususan mashairi pamoja na video. Pale nyimbo zitakapokwenda kinyume na uadilifu zifungwe kwa

sababu binadamu anachokisikia na kukitazama huathiri mienendo yake (Newman, 1980).

**Marejeleo**

BBC News Swahili. (2015). *Muziki wa singeli washika kasi nchini Tanzania*. Kinapatikana katika https://www.bbc.com/swahili/habari-37135137. Kilisikilizwa tarehe 22 Juni 2019.

Bevilaqua, J., Kolovos, M.E. Melman, J. & Hughes, K. (2010). *Haki za Wanawake Tanzania*. Leitner Centre for International Law and Justice: New York.

Dogo Zero na Sniper (2018). “Utanikumbuka. Tanzania”. Ilisikilizwa katika https://www.youtube.com/watch?v=eIrYypeHbyE tarehe 02 Aprili 2022.

Gicuku, M. (2011). Usawiri wa Maudhui ya Ndoa katika Ushairi wa Euphrase Kezilahabi na Kithaka Wa Mberia. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Nairobi, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Gwako, J, B. (2016). Uchanganuzi Linganishi wa Suala la Maadili kwa Vijana wa Kiume katika Tenzi Mbili: Siraji Na Adili. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Nairobi, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Jilala, H. (2016). “Muziki wa Hip Hop na Haki za Kijamii: Dhima, Changamoto Na Mapendekezo”. *Huria: Journal of the Open University of Tanzania*. Juz. 21(1).

King‟ei, G. K. (1992). Culture and Communication: The Role of Kiswahili Taarab Songs in Kenya from 1963-1990. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Cambridge, Havard University.

Kisanji, J. A. N. (2013). Kufuwawa wa Miiko na Kupotoka kwa Maadili: Uchunguzi Kifani Wa Jamii Ya Wabungu. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Tanzania, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kunhiyop, S.Y. (2008). *African Christian Ethics.* Nairobi: Wordalive Publishers.

Lutta, V. O. & Obiri, J. (2015). “Cyber Crime a Rising Threat for Internet - Based Businesses in Western Region, Kenya”. *International Journal of Scientific and Engineering Research*. Juz. 6(3): 317-377.

Manfongo (2016). “Hainaga Ushemeji”. *Hainaga Ushemeji*. Fatality Music, Tanzania. Ilisikilizwa katika https://www.youtube.com/watch?v=gkLL3AJ5Y_I tarehe 02 Aprili 2022.

Massoud, I. A. E. (2018). Kuchunguza Nafasi ya Mwanamke katika Tamthiliya ya Alikiona. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania.

Meja kunta na D voice (2021). “Madanga ya Mke wangu”. Ilisikilizwa katika https://www.youtube.com/watch?v=NaPt97DwWzY tarehe 02 Aprili 2022.

Meja Kunta na Lavalava. (2020). “Wanga. Tanzania”. Ilisikilizwa katika https://www.youtube.com/watch?v=SV1ra6fchW0 tarehe 02 Aprili 2022.

Michuzi, O. (2021). “Meja Kunta awaomba wasanii wa Singeli kuumiza kichwa kutunga nyimbo zenye kujenga jamii”. Mtaa kwa mtaa Blog. Inapatikana katika http://www.mtaakwamtaa.co.tz/2019/08/meja-kunta-awaomba-wasanii-wa-singeli.html. Ilisomwa tarehe 26 Juni 2021.

Mwita, A. (2020). “Hivi muziki ni nini hasa”. Mtayarishaji Blog. Inapatikana katika https://mtayarishaji.blogspot.com/2012/07/hivi-muziki-ni-nini-hasa.html. Ilisomwa tarehe 16 Aprili 2020.

Neuman, S. B. (1980). “Listening Behauviour and Television Viewing”. *The Journal of Educational Research*. Juz. 74(1):15-18.

Neves, M. P. (2016). “Ethics: Ethics as a Philosophical Discipline. Henk ten Have: Encyclopedia of Global Bioethics”. Inapatikana katika https://www.researchgate.net/profile/Maria-PatraoNeves/publication/314282053_Ethics_as_a_philosophical_discipline/links/59ad3080f7e9b9d44cfdc5b/Ethicssaphilosophicaldiscipline.pdf?origin=publication_detail. Ilisomwa tarehe 02 Aprili 2022.

Ngugi, B. M. (2014). Umilisi wa Stadi za Maamkizi katika Ujifunzaji wa Kiswahili. Tasinifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Ngugi, P. M. Y. (2000). “Nafasi ya Muziki Uliopendwa katika Fasihi ya Kiswahili”. *Swahili Forum.* VII, 145-152.

United Nations. (2019). *Sustainable Development Goals Report 2019*. UN: New York.

Zahoro, S. (2018). Vionjo vya Fasihi ya Kisasa ya Kiswahili katika Nyimbo Teule za Kiswahili. Tasinifu ya MA Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.